



Uteuzi na Uwiano wa Maneno Katika Methali: Mfano wa Methali za Kiswahili Zinazorejelea Uhusiano wa Kiudugu

Sauda Uba Juma

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Dar es Salaam Tanzania

Corresponding author: chudam017@gmail.com

Article History:

Received: 30 Sept 2024

Accepted: 13 June 2025

Published: 26 Dec 2025

Maneno muhimu: akisi, methali, muktadha, uamilifu, uteuzi na uwiano

This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license



Ikisiri

Utafiti huu wa kiisimu unalenga kubainisha na kufafanua jinsi uteuzi wa maneno unavyowiana na kushikamana katika methali za Kiswahili. Aidha, utafiti huu unachunguza muktadha na uamilifu wa uteuzi wa maneno hayo katika kuakisi matumizi ya methali za Kiswahili zinazorejelea uhusiano wa kiudugu. Utafiti huu ni matokeo ya data za uwandani za usaili na ushuhudiaji. Mbinu zote hizo kwa pamoja zimemsaidia mtafiti kupata data tosholevu za kujibu lengo la makala hii. Makala hii, imeongozwa na Nadharia ya Mahusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1995). Katika nadharia hiyo mbali na mambo mengine, inazungumzia namna maneno yanavyohusiana katika tungo hadi kupata maana iliyokusudiwa na msemaji kwa msikilizaji. Vilevile, katika makala hii data zimewasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Kwa ujumla, matokeo ya uchunguzi yameweka bayana uteuzi na uhusiano wa maneno kwa lengo la kuakisi uamilifu wa methali hizo za Kiswahili kulingana na muktadha husika. Hivyo, tunapendekeza watafiti wengine wafanye ulinganishi wa methali za Kiswahili na methali za lugha nyingine za Kiafrika. Ulinganishi ambao utaangazia suala la uteuzi na uwiano wa maneno pamoja na uamilifu uliomo katika methali mbalimbali za Kiswahili na lugha za Kiafrika.

Selection and Correlation of Words in Proverbs: A Case Study of Swahili Proverbs Referencing Sibling Relationships

Abstract

This linguistic study aims to identify and explain how word selection correlates and connects in Swahili proverbs. Additionally, this research examines the context and validity of the word selection in reflecting the usage of Swahili proverbs related to sibling relationships. This study is based on field data from interviews and testimonies. These methods collectively helped the researcher obtain substantial data to address the purpose of this article. The article is guided by the Theory of Relevance established by Sperber and Wilson (1995). In this theory, among other things, it discusses how words relate within texts to achieve the intended meaning from the speaker to the listener. Furthermore, in this article, data is presented using an analytical framework. Overall, the findings of the investigation clarify the selection and relationship of words to reflect the validity of these Swahili proverbs according to the relevant context. Therefore, we recommend that other researchers conduct a comparison of Swahili proverbs with proverbs from other African languages. This comparison should focus on the issue of selection and correlation of words, as well as the validity present in various Swahili proverbs and African languages.

Keywords: Reflection, Proverbs, Context, Validity, Selection and Correlation.

1. Utangulizi

Wataalamu mbalimbali wanaeleza kwamba uteuzi wa maneno unakwenda bega kwa bega na maaana iliyokusudiwa msemaji katika tungo kulingana na muktadha wa mazungumzo katika jamii. Binyanya (2014) anafafanua kwamba, uchaguzi wa maneno na muktadha wa mazungumzo humwezesha mzungumzaji kuchagua mada husika na kutumia lugha kwa namna inayoakisi muktadha huo. Nao Msanjila na wenzake, (2011) wanasema kwamba isimujamii inafafanua matumizi ya lugha yanayotegemea mada ya mazungumzo, uhusiano wa wazungumzaji na mahali pa mazungumzo. Maelezo hayo ya Msanjila na wenzake, yanaonesha kwamba, muktadha na watu wanaohusika katika mazungumzo ni muhimu sana katika kukamilisha mchakato mzima wa mawasiliano mwafaka. Aidha, muktadha wa mazungumzo humwezesha msemaji kuchagua mada faafu na kuitumia lugha kulingana na muktadha husika. Ili kupata maana iliyokusudiwa na msemaji katika mawasiliano uteuzi na uhusiano wa maneno katika tungo, ni muhimu ili kukamilisha lengo lilokusudiwa katika mawasiliano hayo. Hivyo basi, endapo maneno

yaliyotumika katika mawasiliano ya msemaji kwa msikilizaji hayatashikamana na kuwiana vizuri katika tungo, bila shaka lengo la mazungumzo halitafikiwa. Maneno ni namna mtu anavyosema (matamshi) katika lugha (BAKIZA, 2010). Maneno hayo huwa anayo kila mzawa yeyote wa lugha husika ambapo huweza kuyateua, kuyatumia na kuyapanga ili yahusiane na kushikamana vema kwa mawanda mapana katika tungo za lugha yake.

Chomsky (2002) anadai kuwa uhusiano na uwiano wa maneno ni muhimu katika lugha ukiyahusisha na namna yanavyounda maana na jinsi maana hizo zinavyotumika katika tungo kulingana na miktadha mbalimbali. Hivyo, uteuzi wa maneno katika tungo unaweza kutofautiana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine. Chomsky anazidi kusesitiza kwamba maneno ni muhimu katika kujenga tungo na kuelewa lugha na namna muundo wa lugha unavyotegemea matumizi sahihi ya maneno. Hivyo, maneno ni hazina ambayo mzungumzaji wa lugha anaweza kuidhibiti. Hii ina maana kwamba kila mzawa wa lugha anao uwezo wa kuteua maneno na kuyaweka katika uwiano na mshikamano unaokubalika katika uundaji wa tungo za lugha yake. Naye Mukhwana (2011) anaeleza kwamba ikiwa mtu yeyote anataka kuwa na utaalumu fulani hana budi kuwa na hazina kubwa ya maneno katika taaluma anayoishughulikia. Maelezo ya wataalamu hao yanatilia maanani umuhimu wa uteuzi maneno katika tungo kwa mzungumzaji wa lugha husika. Kwa ujumla maelezo ya wataalamu hao yanadhirisha wazi kuwa suala la uteuzi na uwiano wa maneno ili kuunda tungo zenye maana katika lugha ni jambo la msingi. Hivyo, uteuzi na uwiano huo wa maneno katika lugha fulani pamoja na uhusiano wake kulingana na muktadha unaotumika, wakati mwingine unaweza kumsaidia anayejifunza lugha ngeni, kuipata lugha hiyo kwa wepesi zaidi.

Uteuzi wa maneno unaweza kuangaziwa pia katika methali za Kiswahili. Methali ni mojawapo ya semi ambazo zinaweza kuwa na matumizi ya namna mbalimbali kulingana na muktadha yalimotumika (Sito, 2015). Kwa ujumla, kazi za wataalamu zinaonyesha wazi kuwa methali ni muhimu sana katika jamii na hivyo ni muhimu kuzichunguza kutokana na uamilifu wake mkubwa. Kwa mujibu wa Mulokozi (1989), methali ni semi fupifupi zenye kueleza kwa muhutasari fikra au mafunzo mazito yanayotokana na uzoefu wa kijamii. Katika jamii mawazo hayo huelezwa kwa kutumia sitiari au mafumbo. Naye Senkoro (2011) anasema kuwa methali ni sehemu ya lugha ambayo inaweza kufananishwa na kiungo cha lugha na kitoweo cha lugha pia. Kiungo hicho hutumiwa kwa kuyatafakari na kuyapima maisha, kufunzia jumuiya na kutawalia jamii na mazingira ya binadamu.

Methali zinaweza kutokana na vyanzo maalumu kulingana na jamii husika. Kuna methali zinazoweza kutokana na hali au mazingira ya sehemu fulani. Aidha, kuna baadhi ya methali zilizopatikana kutokana na ngano. Jascah na Anthony (2018), wanadai kuwa jamii ya Wanandi, baadhi ya methali zao zinatokana na ngano. Ngano hizo zilikuwa ni visa vilivyotambwa kwa watoto wadogo usiku kabla ya kulala. Mara nyingi visa hivyo vilitangulizwa na vitendawili ambavyo watoto walivitegua. Jambo hilo lilifanywa na mabibi au mababu ili kutia shime na kuteka hisia na kumbukumbu zao kabla ya kutambiwa hadithi. Hivyo, mafunzo ya hadithi yanayofumbwa ndiyo yaliyotungiwa methali. Methali hizo, zilikuwa na ujumbe kama kuitanabahisha jamii, kuonya au hata kuadilisha. Si kusudi la utafiti huu kujiingiza kwa kina katika uchunguzi wa methali kwa ujumla. Usuli uliotolewa hapo juu una lengo la kumpatia msomaji walau mwanga kidogo wa kuelewa dhana ya methali kwa ujumla ikiwa ni kipengele kilicholengwa katika makala hii. Hivyo, katika utafiti huu tumechunguza uteuzi na uwiano wa maneno katika methali za Kiswahili. Kwa kuwa methali za Kiswahili ziko nyingi, uchunguzi huu ni mahususi kwa zile tu zinazorejelea uhusiano wa kiudugu pekee. Lengo likiwa ni kutaka kubaini je maneno yaliyoteuliwa katika methali hizo yameshikamana na kuwiana barabara ili kusadifu uamilifu wake katika muktadha husika kwa jamii ya Waswahili au la?

2. Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Mahusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1995). Inaelezwa katika Nadharia hii kwamba tamko lolote linapoelekezwa kwa msikilizaji huwa na lengo la mahusiano yake. Kauli hii ina maana kwamba mzungumzaji anapotamka neno, wakati huohuo msikilizaji anaelewa lengo la msemaji kwa kutumia maneno aliyomua kuyateua pamoja na muktadha uliotumika. Katika Nadharia ya Mahusiano, utambuzi ambao umo akilini mwa binadamu ni muhimu katika kuelewa lugha yake kupitia uteuzi na uwiano wa maneno katika tungo ili kufanikisha mchakato wa mawasiliano. Mathalani, msikilizaji anapoisikia methali ya Kiswahili inayorejelea uhusiano wa kiudugu, popote pale alipo ataweza kuichanganua methali hiyo kwa mujibu wa mwegamo wa kimuktadha uliolengwa na uteuzi wa maneno yaliyotumika katika methali hizo. Hivyo, katika Nadharia ya Mahusiano, msikilizaji anaweza kukisia lengo la msemaji kwa kuzingatia muktadha wa mawasiliano. Kwa mantiki hiyo, msikilizaji anapopata lengo la msemaji kwa kile alichokikusudia inakuwa rahisi kwake kueleweka. Kwa ujumla baadhi ya misingi ya Nadharia hii ni kama ifuatayo: Mosi, Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kuchagua maneno faafu ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa mujibu wa waasisi wa nadharia hii, maneno tofauti yanaweza kuleta maana tofauti na hisia tofauti kwa msemaji au msikilizaji. Pili, Nadharia hii inasisitiza jinsi maneno yanavyohusiana

katika tungo. Hii ina maana kwamba uhusiano huo wa maneno unahusisha sheria na kanuni za kisarufi ikiwa ni pamoja na miundo ya lugha ili kukamilisha mchakato wa mwasiliano. Tatu, Nadharia hii pia imezingatia suala la muktadha wa matumizi ya maneno yanayotumiwa katika tungo mbalimbali. Kwani maana ya neno inaweza kubadilika katika tungo kulingana na muktadha ambao neno hilo limetumika. Nne, Nadharia hii vilevile imeangazia jinsi uteuzi na uhusiano wa maneno unavyoweza kuathiri ujumbe uliokusudiwa katika tungo. Kinachosisitizwa hapa ni kwamba, maneno chanya yanaweza kuhamasisha jambo fulani wakati maneno hasi yanaweza kuathiri maudhui ya tungo. Misingi ya Nadharia hii imetumika katika uchunguzi wa uteuzi na uwiano wa maneno pamoja na uamilifu wake katika muktadha maalumu wa methali za Kiswahili zinazorejelea uhusiano wa kiudugu.

Katika makala hii Nadharia ya Mahusiano imeongoza vema utafiti huu, kwa kuwa mbali na mambo mengine, methali ina kusudi maalumu katika mawasiliano ya jamii kulingana na muktadha wa mawasiliano hayo. Aidha, Nadharia hii imetuongoza katika ufafanuzi wa uteuzi na uwiano wa maneno yaliotumiwa katika methali za Kiswahili zinazorejelea uhusiano wa kiudugu. Hii ni kwa sababu uteuzi wa maneno hayo na uwiano wake ndiyo unaokamilisha lengo lilokusudiwa. Kwa mnasaba huo, Nadharia hii imetuongoza katika ufafanuzi na uhusiano huo wa maneno pamoja na uamilifu wake kulingana na muktadha wa matumizi wa methali hizo kwa jamii ya Waswahili.

3. Methodolojia

Makala hii imetokana na utafiti wa uwandani uliofanyika katika Kisiwa cha Unguja na Pemba. Data zilikusanywa kuanzia mwezi Octoba hadi Novemba 2024. Maeneo yalilohusishwa na utafiti huu kwa upande wa Kisiwa cha Unguja ni kijiji cha Donge na Mkokotoni vilivyopo katika Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kisiwani Pemba, utafiti huu ulifanyika maeneo ya Kuukuu na Makoongwe. Vijiji hivyo viko katika Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika kuipata sampuli ya watoataarifa 40 ambao ni wazee waliohusishwa katika utafiti huu. Sampuli hiyo ilipatikana kupitia watafiti wasaidizi 4 ambao ni wenyeji wa maeneo ya utafiti huu. Aidha, utafiti huu ulihusisha zaidi wazee kwa kuwa tuliadini kwamba, ndio wenye welewa zaidi wa kuzitambua methali za Kiswahili kuliko vijana. Hivyo, sampuli hiyo ya watoataarifa 40 iliyoteuliwa ilitosha kuwakilisha wazee wengine wanaoishi katika maeneo mbalimbali ya Kisiwa cha Unguja na Pemba. Hii inatokana na ukweli kwamba sampuli haipaswi kuwa kubwa sana wala finyu sana bali inapaswa kuwa toshelevu (Sigh 2006; Garg na Kothari 2016). Aidha, data za makala hii zilipatikana kwa

kutumia mbinu ya ushuhudiaji na usaili. Kupitia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti aliweza kuona jinsi wazee hao wanavyozitamka na kuzitumia methali hizo kwa madhumuni maalumu. Vilevile, mbinu ya usaili ilitumika kwa wazee wachache waliokusudiwa kwa minajili ya kutoa taarifa zilizohitajika katika utafiti huu. Data zilizokusanywa kupitia mbinu hizo kwa pamoja zilifanikisha kufikia lengo mahususi la makala hii.

Mkabala wa kitaamuli umezingatiwa katika uchunguzi na uchakataji wa matokeo ya utafiti huu, kwa kuwa matokeo ya makala hii yamewasilishwa kwa njia ya maelezo zaidi kuliko matumizi ya kihesabu au takwimu. Kwa kuzingatia hilo, data za matokeo haya zilizokusanywa kutoka uwandani kupitia mbinu ya ushuhudiaji na usaili ndizo zilizotumika katika upatikanaji wa methali za Kiswahili. Methali hizo, zinatumiwa na Waswahili katika maeneo mbalimbali ya Kisiwa cha Unguja na Pemba. Methali zinazohusu uhusiano wa kiudugu ndizo zilizotafitiwa ili kubaini uteuzi na uwiano wa maneno katika methali hizo. Aidha, kubaini uamilifu wa methali hizo katika muktadha mahususi wa matumizi yake. Udugu uliokusudiwa katika methali hizo ni ule wa kuzaliwa tumbo moja au udugu unaotokana na watu wenye nasaba moja. Hivyo, methali saba (7) kati ya nyingi zilizokusanywa ziliteuliwa na kutumika kama sampuli katika mjadala huu ili kushadidia kile kilicholengwa katika utafiti huu. Ikumbukwe kwamba methali zinazotumiwa na Waswahili ni nyingi mno hata hivyo, sio methali zote zinazotumiwa zinahusu uhusiano wa kiudugu. Hivyo, uteuzi wa methali hizo ulizingatia zaidi uhusiano huo. Kwa jumla, uwasilishaji wa matokeo yaliyopatikana ulihusisha data zilizopatikana, taarifa mbalimbali za kitafiti, pamoja na Nadharia ya Mahusiano.

4. Uchambuzi wa data, Mjadala wa Matokeo

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza namna uteuzi na uwiano wa maneno unavyohusiana na kushikamana ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa katika muundo wa methali za Kiswahili. Mwegamo wa uchunguzi huo, ulijikita katika methali mahususi za Kiswahili ambazo zinarejelea uhusiano wa kiudugu. Kwa kutumia njia ya usaili na ushuhudiaji, watoa taarifa waliolengwa, walibainisha aina mbalimbali ya methali za Kiswahili walizozikumbuka wao wenyewe. Mtafiti alizisikiliza zote na kuzirikodi kwa kutumia kinas sauti na hatimaye kuzinukuu katika shajara. Baadaye, alizichuja zile tu ambazo zinahitajika katika kufanikisha lengo la makala hii. Hata hivyo, katika mchakato wa usaili wakati mwingine mtafiti aliwaongoza watoa taarifa kwa mwelekeo wa kupata data halisi za kujibu lengo la utafi huu. Mtafiti aliendelea kuuliza maswali ya uchokozi ambayo alihisi yangeweza kumsaidia kupata data alizozihitaji. Maswali aliyowauliza watoa tarifa yalikuwa na mwelekeo wa aina nne.

Moja, naomba unitajie methali ambazo zinazungumzia kuhusu uhusiano wa ndugu. Pili, ni maneno yapi katika methali hiyo yanaonesha uhusiano wa ndugu? Tatu, nini maana ya maneno hayo? Nne, methali hiyo inatoa ujumbe gani kwa jamii? Kupitia maswali hayo chokozi, majibu mbalimbali yalitolewa na watoa tarifa kulingana na mtazamo wao. Aidha, mtafiti aliweza kuuliza tena maswali mengine madogo madogo yaliyoibuka baada ya kupata majibu ya awali. Kwa ujumla maswali yaliyoulizwa na mtafiti yalikuwa ni dira ya kupata data stahiki za kukamilisha lengo la makala hii. Hivyo, matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa kuzingatia aina ya methali za Kiswahili zilizolengwa katika kazi hii kama zinavyofafanuliwa katika Jedwali Na. 1 lifuatalo:

Jedwali Na. 1: Orodha ya Methali Zilizotumika katika Utafiti

Na.	Mifano ya Methali Zinazorejelea Uhusiano wa Kiudugu
1.	<i>Damu ni nzito kuliko maji</i>
2.	<i>Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe</i>
3.	<i>Mwana kidonda mjukuu kovu</i>
4.	<i>Mtegemea cha ndugu hufa masikini</i>
5.	<i>Ndugu mtambile usimkalile</i>
6.	<i>Ndugu wakigombana chukua jembe ukalime wakipatana chukua kapu ukavune</i>
7.	<i>Udugu si kufanana bali ni kufaana</i>

Data ya Uwandani (2024)

Katika Jedwali Na. 1 hapo juu, methali isemayo *Damu ni nzito kuliko maji*, inaonesha kuwa kuna uteuzi na uwiano wa maneno mwafaka amabavo yamechanuza maana iliyokusudiwa katika methali hiyo. Mathalani, damu ni msamiati maarufu na muhimu sana kwani ndiyo uhai wa kila kiumbe. Mtu akikosa damu hawezi kuishi ndiyo maana mgonjwa akipungukiwa na damu, mara nyingi daktari anashauri mgojwa huyo aongezewe damu kwa haraka. *Damu* ni majimaji mekundu yaliyomo ndani ya mwili wa mnyama na wadudu wengine mbalimbali. *Kamusi ya Kiswahili sanifu Toleo la 4* (2019) inaeleza kwamba damu ni kioevu kinachopatikana katika mwili wa

wanyama na binadamu, kinachochochea oksijeni, virutubisho na kutoa taka za seli. Aidha, neno *maji* si geni kwa kila mtu popote alipo duniani. Katika *Kamusi hiyohiyo ya Kiswahili Sanifu toleo la 4* inasema kwamba, *maji* ni kioevu kisicho na ladha, rangi au harufu ambacho kinakamilisha maisha. Maji ni muhimu kwa mimea, wanyama na binadamu na pia hutokana na mvua katika bahari, maziwa mito na kadhalika. Kioevu hicho hutumika katika kupikia, kunywa, kuogea na shughuli nyingine nyingi. Katika methali hiyo pia limetumika neno *nzito*. Neno hilo linatokana na neno *-zito* ambalo kinyume chake ni *-pesi*. Kamusi ya *Kiingereza-Kiswahili Toleo la Tatu* (2006) imefasiliwa neno *-zito* kwa namna tofauti kama ifuatavyo: Mosi, uzani uliozidi uwezo wa mchukuaji. Pili, *-enye* tabia zisizochukulika kwa mfano *kiumbe ni mzito*. Hivyo, maneno *damu* na *maji* kama yalivyoteuliwa na kutumika katika methali hiyo yameakisi vema umuhimu wake katika kuleta uamilifu wa methali hiyo kwa jamii ya Waswahili.

Kwa hakika maneno *damu* na *maji* ambayo yameteuliwa katika methali isemayo *damu ni nzito kuliko maji* hayakuteuliwa kinasibu. Maneno hayo yamesadifu barabara lengo la methali hiyo. Aidha, tunabaini namna ambavyo maneno hayo yamelinganishwa uzito wake na hatimaye ikagundulika kwamba *damu* ni *nzito* zaidi ikilinganishwa na *maji*. Hata katika mazingira ya kawaida, tukiiangalia *damu* inaonekana kuwa *nzito* zaidi ya *maji*. Hivyo, maneno hayo yaliyotumika katika mazingira ya kawaida yameteuliwa na kuhaulishwa katika methali hiyo ili kutoa uamilifu unaofaa. Hivyo, moja kwa moja mchango wa muktadha katika uteuzi wa maneno uliotumika katika methali hiyo, unajitokeza waziwazi. Hata hivyo, mazingira ambayo yametumika maneno hayo katika methali hiyo, ni tofauti na yale ya kawaida. Katika mazingira ya kawaida, kila mtu anajua *damu* ni ipi na *maji* ni yepi. Ulinganishi wa maneno *damu* na *maji* katika methali zinazorejelea uhusiano wa kidugu, umetumika katika muktadha wa methali hiyo kwa lengo mahususi. Katika muktadha huo uzito wa *damu*, umechukuliwa sawa na ndugu wa kuzaliwa tumbo moja au ndugu wa karibu. Neno *maji* kama lilivyotumiwa katika muktadha wa methali hiyo, limehusishwa na mtu baki au rafiki ambaye ni mwepesi na hana uzito kama ndugu wa *damu*. Hivyo, neno *damu*, *nzito*, *kuliko* na *maji* yameoana vyema na muktadha wake, kwa kuwa uteuzi wa maneno hayo ni mwafaka katika methali hii. Hivyo, kwa mujibu wa misingi ya Nadharia ya Mahusiano ambayo imeongoza utafiti huu, inayosema kwamba ni muhimu kuteua maneno faafu ambayo yataonesha uamilifu wake katika muktadha mahususi ili kufikisha lengo lililokusudiwa kwa jamii. Kwa misingi hiyo, uteuzi na uwiano wa maneno hayo unaonesha kwamba, uhusiano wa kidugu ni muhimu au bora zaidi kuliko uhusiano wa mbali. Tuchunguze methali nyingine kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 hapo juu:

Katika methali isemayo *mila nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe*, kuna maneno ambayo yameteuliwa na yanaonekana kuwiana na kushikana vizuri katika mundo wa methali hiyo. *Mila* ni neno linalorejelea nomino ya mazoea ya mtu anayefanya kitendo cha kula (anayekula). Mofu //m- imesetiri nomino ambayo ni mtu na kitenzi kinachofanywa na mtu huyo ambacho ni kula. Neno *hafi* ni kitenzi cha ukanushi ambacho pia hurejelea mazoea. Kwa upande wa neno *nawe* nalo linamrejelea mtu ambapo neno hilo, nimeunganishwa na kiunganishi *na* pamoja na kiwakilishi *wewe*. Kiwakilishi hicho, kinawakilisha nafsi ya pili umoja. Hali kadhalika neno *mzaliwa* lina maana mtu aliyetoka na mwenzake katika tumbo la mama au baba mmoja. Hivyo, uhusiano uliopo kati ya maneno hayo, unafaa katika muktadha wa methali hiyo inayorejelea uhusiano wa kiudugu. Sote tuna ufahamu fika kuwa maneno hayo ni muhimu sana tunapowaelezea watu ambao wana udugu wa damu. Ndugu yako wa damu ndiye pekee ambaye mtaishi, mtakufa na na wala sio mtu wa mbali (asiyekuwa ndugu yako). Mtu ambaye si ndugu yako, munaweza kuishi pamoja, mukala pamoja ila sio lazima mufe pamoja. Inawezekana kabisa watu wakajenga urafiki mzuri tu na watu wa mbali ila baada ya muda fulani, uhusiano huo unaweza kupotea. Uhusiano wa kiudugu hauishi wala haupotei ni wa milele, watake au wasitake wao ni ndugu tu. Hivyo, maneno *mila*, *nawe*, *hafi* na *mzaliwa* yamekidhi vigezo vya kuteuliwa na kuwiana kwake katika methali hiyo. Hii ni kudhihirisha kile kisemwacho katika Nadharia ya Mahusiano iliyotumika katika makala hii kwamba, uteuzi na uhusiano wa maneno na mshikamano wake, unavyoweza kuathiri ujumbe uliokusudiwa katika tungo kulingana na muktadha uliotumika. Tuchunguze methali ifuatayo iliyomo katika Jedwali Na.1:

Mwana kidonda mjukuu kovu Methali hii nayo ni miongoni mwa methali zinazorejelea uhusiano wa kiudugu. Maneno yaliyoteuliwa ni *mwana*, *kidonda*, *mjukuu* na *kovu*. Kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010) maneno yamefafanuliwa kimtawalia kama ifuatavyo: *mwana* ni kiumbe kilichozaliwa na binadamu au mnyama pia mtoto. Vilevile, *mwana* ni neno la heshima linalotumika kabla ya kutaja jina la mwanamke kama vile Siti, Nunu na Fatuma (mwanafatuma). *Kidonda* ni sehemu ya mwili iliyoumia kama vile kwa kujikata, kuchunika au kuungua pia *kijeraha*. Ama kuhusu neno *mjukuu* kwa mujibu wa Kamusi hiyo, inaeleza kuwa ni mwana wa kiume au kike wa mtoto wake mtu. Kwa upande wake neno *kovu* linaelezwa kwamba ni ile alama iliyobaki baada ya kidonda kupoa. Katika methali hiyo, Uteuzi huu wa maneno *mwana*, *kidonda*, *mjukuu* na *kovu*, unasawiri ukweli wa kimuktadha katika uhalisia wa maisha ya jamii ya Waswahili. Muktadha

ambao, unakwenda sanjari na uteuzi, uhusiano na mshikamano wa maneno yake. Hivyo, uhusiano wa kiudugu umejitokeza dhahiri katika methali hiyo.

Tukiyachunguza kwa makini maneno hayo, tunagundua kwamba uhusiano wake ni ule wa mtoto na mzazi wake. Kwa kawaida katika jamii yoyote iwayo *mwana* huwa ndicho *kidonda* na *mjukuu* ndiye *kovu*. Hii ina maana kwamba mtoto wako wa kumzaa anauma zaidi kuliko mtoto wa mtoto wako (mjukuu). Uhusiano wa maneno hayo ni kwamba, *kidonda* kinauma zaidi na mtu akiwa nacho huwa hataki kiguswe na kitu chochote kutokana na maumivu yake. Hata hivyo, *kidonda* inapopona kinabaki *kovu*. *Kovu* ambayo mtu yeyote anaweza kuishika na wakati mwingine bila kuhisi maumivu yoyote. *Kovu* hiyo ndiyo inayohusianishwa na *mjukuu* kwa kuwa maumivu ya mtoto ni makubwa zaidi kuliko ya *mjukuu*. Pamoja na ukweli huo wakati mwingine huenda mambo yasiwe kama tunavyofikiria na kuonekana kinyume cha matarajio ya watu. Hivyo basi, ingawa uteuzi wa maneno hayo umedhihirisha ukweli wa maisha kwamba kila binadamu ana maumivu na mtoto wake aliyemzaa. Hata hivyo, wakati mwingine maisha huwa yanabadilika kutokana na matendo, mitazamo, tajiriba na mielekeo ya watu. Hivyo, huenda tukakumbana na hali ambazo ni kinyume cha matarajio ya watu kutegemea muktadha na mahusiano ya viumbe husika katika mazingira yao halisi. Tuanaona mifano mbalimbali katika jamii ambapo mtu anaweza kumuua mtoto wake au akapenda zaidi *mjukuu* wake kuliko mtoto wake wa kumzaa. Hata hivyo, hali kama hiyo ya kumpenda *mjukuu* huweza kujitokeza kwa nadra kulingana na mitazamo na mitagusano ya baadhi ya watu. Kiuhalisia mtoto anauma zaidi kuliko *mjuu*. Uteuzi na uhusiano huo wa maneno umezingatia misingi ya Nadharia ya Mahusiano iliyouongoza utafiti huu. Maneno yanateuliwa na kuhusiana vizuri kwa mujibu wa muktadha yaliyotumika maneno hayo ili kufikisha ujumbe kwa jamii lengwa. Methali nyingine inayodokeza uhusiano wa kiudugu ni:

Mtegemea cha ndugu hufa masikini ni miongoni mwa methali za Kiswahili. Katika methali hii, neno *mtegemea* limeundwa na mofu kadhaa hata hivyo tumezingatia kile ambacho kinahusika tu katika uchambuzi huu. Neno hilo lina mofu //m-// na //tegemea//, mofu {m} inamwakilisha mtu na //tegeme-a// ni mofu mbili ambazo zinaonesha kitenzi. Mofu hizo zimeungana kwa pamoja na kuunda neno *mtegemea* ambalo linawakilisha mtu ambaye ni nomino. Hivyo, sifa na uhusiano wa uteuzi wa maneno hayo unakamilisha lengo la methali hiyo. Katika jamii kila mtu anatakiwa kupambana ili apate cha kwake. Endapo mtu atalemaa na kumtegemea jamaa yake atakufa masikini. Hivyo, uhusiano wa maneno hayo unatoa angalizo kwamba, binadamu tumeumbwa katika familia mbalimbali zenye uhusiano kinasaba. Hata

hivyo, kila mmoja katika ukoo ana familia yake inayomtegemea. Mathalani, kila ndugu ana mke na watoto wake ambao ndio wategemezi wake. Katika maelezo haya tunaona jinsi muktadha ambao maneno hayo yametumika, unavyowiana na maneno *ndugu*, *hufa* na *maskini* katika methali hiyo. Uteuzi huo wa maneno unadhihirisha ufanisi mkubwa wa methali hii katika jamii ya Waswahili, kwa kutupa uhusiano na uwiano uliopo baina ya *mtegemea cha ndugu* na *kufa maskini*. Uteuzi na uhusiano huo wa maneno, unathibitisha uhalisia wa Nadharia ya Uhusiano katika mihimili yake kwamba ni muhimu kuchagua maneno yanayofaa na kuhusiana vilivyo katika kuunda tungo zenye uamilifu mbalimbali kulingana na muktadha fulani. Tufuatilie methali nyingine iliyomo katika Jedwali Na. 1 hapo juu:

Mfano mwingine wa methali kama ulivyobainisha katika Jedwali Na. 1 ni ule usemao *ndugu mtambile usimkalile*. Katika methali hiyo, tunapata ufahamu kuhusu namna gani tunaweza kuishi na ndugu vizuri bila kuwepo na ugomvi wa mara kwa mara. Katika baadhi ya jamii za Waswahili, mara kadhaa huweza kuibuka ugomvi wa wenyewe kwa wenyewe. Kuna mambo kadhaa ambayo huweza kusababisha ugomvi huo. Kwa mfano, mali, kuoneana wivu, mafanikio na kadhali. Hata hivyo, katika methali hiyo ugomvi wa ndugu unaorejelewa si kama huo ambao tumeubainisha hapo juu la hashu! Methali hiyo inarejelea ugomvi wa ndugu ambao unaweza kuibuka wakati ndugu hao wanapoamua kuishi au kukaa pamoja kwa muda mrefu. Aidha, methali inadokeza kuwa maelewano ya ndugu katika familia ni kuishi maeneo tofauti. Mara kadhaa katika jamii zetu, tunashuhudia ugomvi wa ndugu kwa sababu zisizo na msingi wowote ule. Hivyo basi, kutokana na sababu hizo, ndiyo maana methali hiyo iliibuka ili kuitahadharisha jamii juu ya suala hilo.

Uteuzi wa maneno *mtambile* na *usimkalile* umeleta uwiano mzuri na neno *ndugu* kutokana na sifa walizonazo baadhi ya ndugu katika jamii zetu. Maneno hayo mawili kwa mujibu wa watoa taarifa katika utafiti huu, yana asili ya lahaja ya Kipemba. Neno *mtambile* maana yake mtembelee na *usimkalile* maana yake usimkalie. Kwa ujumla methali hiyo, inaeleza kwamba ndugu wanatakiwa kutembeleana na sio kuishi mahali pamoja. Methali hii inatoa hekima kubwa kwa kuwa endapo ndugu hawataishi pamoja bali watatembeleana tu, bila shaka kila mmoja atakuwa na hamu au shauku ya kukutana na mwenzake. Jambo hili huenda likawasaidia ndugu hao, kuishi vizuri na kusaidiana kama familia bila kutokea ugomvi wa aina yoyote. Hivyo, uteuzi na uwiano wa maneno *mtambile* na *usimkalile* umehusishwa na neno *ndugu* katika methali hiyo ili kutoa uamilifu wake kulingana na muktadha uliokusudiwa kama inavyofafanuliwa katika Nadharia ya Mahusiano. Uamilifu uliokusudiwa katika methali hiyo ni ule wa kuitanabahisha jamii ili ichukue hadhari ya kuona

namna bora ya kuishi na ndugu bila kugombana.

Katika Jedwali hilohilo Na. 1 kuna methali nyingine inayosema kwamba, *ndugu wakigombana chukua jembe ukalime wakipatana chukua kapu ukavune*. Katika methali hiyo, kuna maneno ya kawaida ambayo yanatumiwa na wazungumzaji wa lugha hii kila uchao. Hata hivyo, katika methali hiyo maneno hayo yameteuliwa na kuwiana vema ili kukidhi madhumuni yaliyolengwa kulingana na muktadha mahususi. Neno kuu katika methali hiyo, ni *ndugu* ambalo linahusishwa na ugomvi na mapatano. Kwa kawaida baadhi ya jamii nyingi za Kiafrika ugomvi wa ndugu ni jambo la kawaida kutokea. Inawezekana kabisa ukatokea ugomvi kwa wanandugu kutokana na sababu za msingi. Mara nyingi, ugomvi wa aina hii unaweza kusababishwa na ndugu mmoja au wawili ambao ni wakorofi katika familia fulani. Aidha, ugomvi huo unaweza kutokea kwa sababu ya mirathi, mali au maslahi yaliyopo, pengine baada ya wazazi kufariki. Kwa upande mwingine, unaweza kuibuka ugomvi katika familia usiokuwa na kichwa wala miguu. Ugomvi ambao hauna sababu kuntu, isipokuwa ni ndugu wenyewe kwa wenyewe ambao hawapendani. Methali hii inaonyesha kwa uwazi tofauti za kitabia zilizopo kati ya binadamu katika mazingira yao. Hivyo, basi tofauti kama hizi zinapotokea kwa wanandugu na kusababisha ugomvi, jamii inapaswa kuchukuwa hadhari kubwa. Mfuatano wa maneno *ndugu wakigombana chukua jembe ukalime*, yanalenga kueleza jamii kwamba wasiingilie ugomvi wa ndugu. Ndugu wanaweza kugombana na wakafikia hadi kupigana ila wanajamii hawapaswi kuwaingilia katika ugomvi wao. Wanajamii wanashauriwa kushughulika na mambo yao na kuendelea na kazi zao za kila kikawaida kama vile za kilimo.

Kauli hii inaakisi ukweli kwamba wakati mwingine, ugomvi wao huwa haudumu kwa muda mrefu. Baada ya muda fulani ndugu hao wanaweza kupatana tena na kuendelea na maisha yao. Hivyo, endapo mtu yeyote atajaribu kuwaingilia anaweza kujikuta ameingia kwenye mtego. Hali hii inaweza kutokea kwa sababu baada ya mapatano ya ndugu hao, yule aliyeingilia ugomvi wao ataonekana ndiye mbaya. Sanjari na hilo, maneno *wakipatana chukua kapu ukavune*, yanasadifu barabara dhima ya methali hii kwa jamii. Baada ya ugomvi kutokea mwanajamii hakuingilia ugomvi na badala yake alikwenda shamba kulima. Aidha, ugomvi unapokwisha baina yao, anachukua kapu na kwenda shamba kuvuna. Hivyo, uteuzi wa maneno *ukalime* na *ukavune* yamekidhi sifa za uteuzi wake katika muktadha wa methali hiyo. Hali hii ya uteuzi huo imetokea kwa sababu, ugomvi wa ndugu umenasibishwa na kulima. Kila mmoja anaelewa kwamba kulima ni kazi ngumu na yenye maumivu na ndiyo maana ikafananishwa na ugomvi. Kama tunavyojua kwamba ugomvi si kitu

kizuri hata kidogo kwa binadamu yeyote yule sembuse ndugu, hivyo ugomvi haufai. Kwa upande mwingine mapatano ya wanandugu nayo yamenasibishwa na uteuzi wa maneno *chukua kapu ukavune*. Hapa bila shaka kinacholengwa ni matunda au mavuno ambayo ni mapatano ya wanandugu hao baada ya ugomvi wao kuisha. Kwa ujumla, katika methali hiyo uteuzi wa maneno yake, umewiana vizuri ili kumamilisha lengo la methali husika kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Mahusiano.

Methali ya mwisho iliyojadiliwa katika Jadweli Na. 1 ni *udugu si kufanana bali ni kufaana*. Kwa kawaida inategemewa kwamba ndugu wa tumbo moja mara nyingi huweza kufanana kwa sura, umbo au hata tabia. Mara kadhaa inatokea unapomwambia mtu huyu ni ndugu yangu anaweza kukuuliza kweli mbona hamufanani? Kufanana au kutofanana kwa ndugu wa tumbo moja kunawezekana lakini sio lazima hilo litokee kwa ndugu hao. Ndugu wanaweza wakafanana au wakatofautiana kulingana na urithi au kudra tu za Mwenyezi Mungu kwa waja wake. Hata hivyo kufanana au kutofautiana kwa wanandugu kimuonekano wa nje sio jambo la msingi wala jambo la lazima. Hayo yote ni maumbile ya kibinadamu kwa kuwa inaweza kutokea, watu wawili ambao hawahusiani kabisa kinasaba na wakaweza kufanana pia. Kinyume chake ndugu wanaweza kuwa wamezaliwa mama mmoja na baba mmoja lakini wakatofautiana kabisa na wakaonekana kama sio ndugu wa tumbo moja. Hivyo, uteuzi na uwiano wa maneno *ndugu, kufanana* na *kufaana* yanarejelea hekima na mafunzo yanayopatikana katika methali hiyo. Kinachosemwa hapo ni kwamba kitu kilicho muhimu na cha msingi zaidi kwa wanandugu ni *kufaana* kwa maana ya kusaidiana kwenye shida na raha. Bila shaka methali hii ina maana kwamba wanandugu wanatakiwa kusaidiana, kuhurumiana, kutembeleana na kushirikiana kwa kila jambo. Ndugu hawatakiwi kabisa kufarakana wala kuonana kama maadui. Ndugu wanatakiwa kuwa kitu kimoja, tatizo la ndugu mmoja linatakiwa liwe ni tatizo la ndugu mwingine pia. Hii ndiyo kusema kwamba sifa za uteuzi na uwiano wa maneno *kufanana* na *kufaana* ambayo yamehusishwa na neno *ndugu*, yameakisi kile kisemwacho katika Nadharia ya Mahusiano. Kama tuvyotangulia kusema kwamba, Nadharia hii inasisitiza uteuzi wa maneno, jinsi maneno hayo yanavyohusiana na kushikamna vizuri, muktadha uliotumika katika tungo ili kufikia lengo la methali hiyo katika uamilifu wake.

5. Hitimisho

Katika utafiti huu tumeshughulikia sifa na uwiano wa uteuzi wa maneno katika methali za Kiswahili zinazorejelea uhusiano wa kiudugu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba maneno katika methali zilizobainishwa katika makala hii, yameteuliwa na kuwiana vema kulingana na kusudio la methali hizo. Aidha,

uchanganuzi huo umeonesha kuwa matumizi ya maneno hayo katika methali za Kiswahili zinazorejelea uhusiano wa kiudugu, huwa na uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu yake katika muktadha mahususi. Hivyo, katika utafiti huu tulibanwa na upeo pamoja na mipaka kwa kuwa tumeshughulikia aina hiyo tu ya methali za Kiswahili. Hata hivyo, taalumu ya methali ni pana na ina mambo mengi yanayoweza kuchunguzwa kwa ujumla wake.

6. Mapendekezo

Pamoja na maelezo hayo, tunapendekeza yafuatayo: Mosi, kufanya uchunguzi wa methali katika makundi mengine mbalimbali ili kupata uelewa wa kina kuhusiana na uteuzi na uwiano wa maneno pamoja na uamilifu wake katika methali za Kiswahili. Utafiti kama huo utatupatia mifano zaidi ya kuona jinsi maneno yanavyoteuliwa, kuwiana na kuhusiana kwa malengo mbalimbali. Pili, kwa kuwa utafiti huu, umejikita katika methali za Kiswahili peke yake, tunapendekeza watafiti wengine wafanye ulinganishi wa methali za Kiswahili na methali za lugha nyingine za Kiafrika. Ulinganishi ambao utaangazia suala la uteuzi na uwiano wa maneno pamoja na uamilifu uliomo katika methali mbalimbali za Kiswahili na lugha za Kiafrika.

Marejeleo

BAKIZA (2010). *Kamusi la Lahaja ya Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press.

Binyanya, M. R. (2014). *Sajili ya Maafisa wa Polisi: Tathmini ya Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Kituo cha Polisi cha Central, Nairobi*. Tasnifu ya Umahiri. [Haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chomsky, N. (2002). *On Nature and Language*. Cambridge University Press.

Garg, G. na Kothari, C.R. (2016). *Research Methodology: Methods and Techniques*. 3rd Edition. New Age International Publishers.

Jescah, N. C. na Anthony, B. K. (2018). Methali katika Jamii ya Wanandi: Chimbuko na Uainishaji wake. *CHAKAMA*, uk 93-107.

Msanjila, Y. P na Wenzake (2011). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi. *Jarida la Mulika*, Na. 21.

Mukhwana, A. (1990). *Siasa na Uimarikaji wa Kiswahili Kenya*. Tasnifu ya Uzamili.

[Haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Senkoro, F. E. M.K. (2011). *Fasihi*. KAUTTU Limited.

Sigh, J. K. (2006). *Fundamental of Research Methodology and Statistics*. New Age International Publishers.

Sito, P. S. (2015). *Athari za Mazingira katika Uteuzi wa Msamiati: Mfano wa Methali za Kiswahili Zinazorejelea Viumbe wa Majini*. Tasnifu ya Umahiri. [Haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sperber D. na Wilson, D. (1995). *Relevance Theory*. Blackwell.

TUKI. (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili (Toleo la Tatu)*. TUKI.

TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la Nne)*. Oxford University Press.